

Jilinde dhidi ya Surua: Pata Ukweli



Idara ya Afya inafuatilia mlipuko wa surua katika Philadelphia. Surua inaweza kuwa hatari, hasa kwa watoto wachanga na watoto wadogo. Inaambukiza zaidi kuliko virusi vingine.

Mara nyingi surua huanza na homa, mafua puanzi, kikohozi, macho mekundu na madoa meupe mdomoni. Siku kadhaa baadaye, upele nyekundu huanza kutoka kwa uso, na kusonga chini kwa mwili wote.

Surua inaweza kusababisha maambukizi makubwa ya mapafu yanayoitwa nimonia, uvimbe wa ubongo unaoitwa encephalitis, madhara ya muda mrefu, kulazwa hospitalini, na kifo.

Je, surua hueneaje?

Surua huenea kwa kuwa karibu na mtu aliye na surua ambaye anakoho, kupiga chafya, au kupumua tu. Surua inaweza kuenea kabla ya mtu aliye na surua kupata upele na baada ya dalili kuisha. Viini vinaweza kudumu ndani ya chumba kwa saa mbili baada ya mtu aliye na surua kuondoka.

Ni kinga gani bora dhidi ya surua?

Kupata chanjo! Mfululizo wa chanjo ya MMR unapendekezwa katika miezi 12-15 na tena mtoto anapofikisha miaka 4. Watoto wachanga walio na umri wa zaidi ya miezi 6 wanapaswa kupata dozi ya chanjo ya MMR kabla ya kusafiri hadi nchi ambako surua ni kawaida zaidi.



Takriban mtu 1 katiki ya 5 anayepata surua atalazwa hospitalini.



Mtu 1 katiki ya kila watu 1,000 walio na surua atapata uvimbe wa ubongo kutoptana na maambukizi (encephalitis), ambayo yanaweza kusababisha uharibifu wa ubongo.



Mtu 1 hadi 3 katiki ya 1,000 walio na surua watakuwa, hata kwa uangalizi bora zaidi.

Tafuta maeneo ya chanjo kwenye ukurasa unaofuata. →

Jilinde dhidi ya Surua: Pata Chanjo



Chanjo ya surua, mabusha na rubela (MMR) ndiyo kinga yako bora dhidi ya surua. Inapatikana bila malipo kwa wakazi wote wa Philadelphia katika kila Kituo cha Afya cha Jiji.

Mtoto yejote katika Philadelphia anaweza kupokea chanjo katika Vituo vya Afya vya Jiji. Piga simu 215-685-2933 ili kuweka miadi.

Kwa muda mfupi:

Vituo vya Afya vya Jiji vitatoa chanjo za MMR kwa wanaoingia kwa mkazi yejote wa Philadelphia, **Jumatatu hadi Ijumaa, Saa 4 Asubuhi - Saa 6 Adhuhuri na Saa 7 mchana - Saa 9 Alasiri.**

Kituo cha Afya 3

555 S 43rd St, Philadelphia, PA 19104

Kituo cha Afya 4

4400 Haverford Ave, Philadelphia, PA 19104

Kituo cha Afya 5

1900 N 20th St, Philadelphia, PA 19121

Hakuna haja ya miadi! Hakuna haja ya kitambulisho, sehemu ya barua tu na anwani yako itafanya kazi!



Kwa taarifa kuhusu mahali pa kupata chanjo ya MMR, tembelea bit.ly/PhilaMeasles. Kwa taarifa kuhusu mlipuko wa surua katika Philadelphia, tembelea bit.ly/Measles2024PHL.